

**TAARIFA YA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM MHE. PAUL
MAKONDA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAPOKEZI YA
MWENGE WA UHURU.**

Mwenge wa uhuru ni chombo kilichoasisiwa na baba wa taifa mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwak 1961 ikia ni Tunu na ishara ya kuwepo kwa Taifa huru la Tanganyika. Mbio za Mwenge wa Uhuru rasmi mwaka 1964 baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa nchi inayoitwa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mbio za Mwenge wa Uhuru tangia mwanzo zimekuwa kichocheo kikubwa katika kuhamasisha Maendeleo , uzalendo, Umoja , Mshikamano na kudumisha Amani ndani na nje ya Taifa letu.

Mwaka huu utakuwa mwaka wa 24 tangu mbio za Mwenge wa Uhuru zirejeshwe chini ya utaratibu wa usimamizi wa serikali. Hii ilitokana na mabadiliko ya kidemokrasia baada ya nchi yetu kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Katika kutimiza adhama iliyowekwa na waasisi wa Taifa hili wakati wa kuanzisha Mbio za Mwenge kama kichocheo kikubwa katika kuhamasisha Maendeleo, uzalendo, Umoja, Mshikamano na kudumisha Amani ndani na nje ya Taifa letu, mkoa wetu wa Dar es salaam utapokea Mwenge wa Uhuru siku ya tarehe 25/05/2017 saa 3 asubuhi kutoka Mkoa wa Lindi katika eneo la Kongowe Shule ya Msingi Kongowe/Mzinga kata ya Tuangoma na kukabidhiwa katika wilaya ya Temeke.

Mwenge huu utakimbizwa katika Mkoa wetu ukizindua miradi mbali mbali ya kimaendeleo kwa utaratibu ufuatao.

Tarehe 27/05/2017 utakimbizwa katika Wilaya ya Temeke.

Tarehe 28/05/2016 utakimbizwa katika Wilaya ya Kigamboni.

Tarehe 29/05/2016 utakimbizwa katika Wilaya ya Ilala.

Tarehe 30/05/2017 utakimbizwa katika Wilaya ya Kinondoni.

Tarehe 31/05/2017 utakimbizwa katika Wilaya ya Ubungo.

Mwenge wa Uhuru utamaliza mbio zake hapa mkoani Dar es salaam siku ya tarehe 31/05/2017 na kukabidhiwa kwa uongozi wa Mkoa wa Pwani siku ya tarehe 01/06/2017 katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Terminal 1 kwa ajiri ya kwenda Mafia Mkoani Pwani.

Natoa wito kwa wakazi wenzangu wa Mkoa wa Dar es salaam kujitokeza kwa wingi kuulaki Mwenge wetu wa Uhuru katika maeneo yote utakao kuwepo ndani ya mkoa huu kwani pamoja na mambo yote ni urithi na nembo ya umoja na maendeleo yetu.

PAUL C. MAKONDA

MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM

26/05/2017.